

# Jinzi ya kuendeleza haya masomo

## Maombi

Wakati wote kumbuka kuomba Mungu. Omba Mungu akusaidie ufundishe watoto vizuri. Pamoja na watoto sema sala mkianza tena baada ya kila somo.

## Kusoma Biblia

Mwanzoni mwa kila somo kuna mistari ya kusoma kutoka kwa Biblia. Wakati mwingine mistari ni mingi. Hizo mistari ni za Mwalimu kusoma ili zimsaidie atayarishe somo. Zitasaidia Mwalimu asome Biblia kwanza. Kutokea hapo Mwalimu atachagua mistari zinazofaa kusomea watoto. Watoto wakubwa wanaweza kusoma mistari michache.

## Kiini cha Somo

Hii inasaidia Mwalimu kuhakikisha kwamba watoto wanapata somo lililo la maana kutoka kwa Biblia.

## Somo

Hapa ni hadithi yenyewe. Inaweza kusomewa watoto au Mwalimu asome pekee yake na imsaidie kufundisha. Mwalimu anaweza kufundisha kwa kinaganaga akirudia au apanue kindani kusaidia watoto waelewe.

## Maswali na Majibu

Kwa kila somo kuna maswali na majibu 10. Haya si maswali pekee ya kuulizwa. Mwalimu anaweza kutengeneza maswali mengine kuuliza watoto. Watoto wakiwa na shida ya kuelewa pahali popote, uliza maswali mengi hapo ili waelewe.

## Ona kwamba haya masomo yanavutia

- Onyesha watoto picha zenye zimepakwa rangi
- Fundisha watoto nyimbo na tenzi
- Fundisha watoto mstari wa kukariri juu ya somo
- Watoto wakubwa wanaweza kuandika habari
- Watoto wanaweza kuchora picha juu ya hiyo hadithi.
- Watoto wajaribu kueleza hiyo hadithi kwa maneno yao au waigize kwa mchezo

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



## Habari kwa Walimu

### Awamu ya 2 Mwaka wa 1

Masomo ya Awamu 2 yanastahili kufunza watoto wenye wanakaribia umri wa miaka 11 – 14. (Masomo ya Awamu 1 ni ya watoto wa umri wa mpaka miaka 10).

Kuna masomo ya miaka miwili kwa Awamu 2. Masomo yote ni 51 kwa mwaka mzima. Kila wiki ina somo moja. Kuna wiki moja la likizo. Masomo haya yafaa kurudiwa mara tena ili yapate kufundishwa kwa miaka 4: yaani miaka 11 – 12 tena miaka 13 -14.

### Somo la miaka miwili

Ni masomo ya miaka miwili. Kuna masomo 51 kwa kila mwaka. Kila juma lina somo moja. Juma moja ni la kupumzika.

Masomo ya mwaka wa 1 yanaanza na uumbaji kwa Bustani ya Edeni katika Agano la Kale. Haya masomo yanaendelea kwa Agano la Kale mpaka kwa Waamuzi. Baadaye kwa Agano Jipya yanaanza na kuzaliwa kwa Yesu mpaka alipopaa kwenda mbinguni.

Mwaka wa 2 masomo yanaendelea kutoka kwa Mwamuzi Samsoni mpaka mwisho wa Agano la Kale. Masomo ya Agano Jipya yanatoka kwa kitabu cha Matendo.

Haya masomo ya miaka miwili yanaweza kurudiwa tena kwa miaka mingine miwili ili watoto wasome na kuelewa vizuri.

# VITABU VYA BIBILIA

## Vichwa vya masomo - Mwaka wa 1

1	Bustani ya Edeni	27	Rahabu na wapelelezi
2	Kaini, Habili na Sethi	28	Watu wa Mungu wanavuka Mto Yordani
3	Nuhu		
4	Mwito wa Abramu	29	Yoshua na vita vya Yeriko
5	Abramu na Lutu	30	Waisraeli washinda Ai
6	Isaka kama dhabihu	31	Debora na Baraka
7	Mke wa Isaka	32	Gideoni apiga Wamidiani
8	Yakobo na Esau	33	Kuzaliwa kwa Yesu
9	Yakobo anafanya Labani kazi	34	Yohana Mbatizaji
10	Yakobo anashindana na malaika	35	Kubatzwa kwa Yesu na majaribu
11	Koti la Yusufu		
12	Yusufu gerezani	36	Yesu achagua wanafunzi 12
13	Ndoto za Farao	37	Mtumishi wa Akida
14	Ndugu Yusufu wanakuja Misri	38	Mfano wa nyumba 2
15	Familia ya Yusufu inakuja Misri	39	Maombi
16	Kuzaliwa kwa Musa	40	Ugeuzi
17	Musa aona kichaka kikichomeka	41	Yesu Alisha watu 5000
18	Musa na tauni kumi	42	Watu kumi wa ukoma
19	Waisraeli wavuka Bahari ya Shamu	43	Mwana mpotevu
20	Waisraeli jangwani	44	Msamaria mwema
21	Amri kumi	45	Martha na Mariamu
22	Ndama ya dhahabu	46	Lazaro afufuliwa kutoka kwa wafu
23	Wapelelezi kumi na mbili	47	Yesu anaingia Yerusalemu
24	Musa apiga mwamba	48	Chakula cha mwisho
25	Nyoka ya shaba	49	Kusulubiwa na kufa kwa Yesu
26	Yoshua kiongozi mpya	50	Yesu anaishi tena
		51	Yesu anaenda Mbinguni

### Sheria

Mwanzo  
Kutoka  
Mambo ya Walawi  
Hesabu  
Kumbukumbu la Torati

### Historia

Yoshua  
Waamuzi  
Ruthu  
1 & 2 Samweli  
1 & 2 Wafalme  
1 & 2 Mambo ya Nyakati  
Ezra  
Nehemia  
Esta

### Injili

Mathayo  
Marko  
Luka  
Yohana

### Matendo

### Agano La kale

### Mashairi

Ayubu  
Zaburi  
Mithali  
Mhubiri  
Wimbo ulio Bora

### Unabii

Isaya	Yona
Yeremia	Mika
Maombolezo	Nahumu
Ezekieli	Habakuki
Danieli	Sefania
Hosea	Hagai
Yoeli	Zekaria
Amosi	Malaki
Obadia	

### Agano jipya

#### Barua za Paulo

Warumi	Wakolosai
1 & 2 Wakorintho	1 & 2 Wathesalonike
Wagalatia	1 & 2 Timotheo
Waefeso	Tito
Wafilipi	Filemoni

#### Barua Zingine

Waebrania  
Yakobo  
1 & 2 Petro  
1, 2, 3 Yohana

### Ufunuo